TANGAZO LA SERIKALI NA. 195 la tarehe 22/3/2023

SHERIA YA HUDUMA ZA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA
(SURA YA 272)

# NOTISI

*(Imetayarishwa chini ya Kifungu cha 9(1) na (2))*

NOTISI YA KUONGEZA ENEO LA HUDUMA ZA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA LA MAMLAKA YA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA TANGA MJINI YA MWAKA 2024

Jina

1. Notisi hii itajulikana kama Notisi ya kuongeza eneo la Huduma la Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Tanga Mjini ya mwaka 2024.

Kuongeza eneo la huduma

2. Eneo la huduma la Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Tanga Mjini limeongezwa kujumuisha eneo lililoainishwa katika Jedwali la Notisi hii.

Kukoma kwa shirika la kijamii au taasisi

3. -(1) Shirika la kijamii au taasisi iliyosajiliwa kutoa huduma za maji na usafi wa mazingira kabla ya kuanza kutumika kwa Notisi hii, katika eneo lililoainishwa katika Jedwali la Notisi hii, itasitisha kutoa huduma hiyo.

(2) Haki, majukumu, ajira za watumishi, mali, madeni na masuala mengine yaliyotolewa au kufanywa na shirika la kijamii la huduma ya maji au taasisi iliyotajwa katika aya ndogo ya (1), yatakuwa chini ya himaya ya Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Tanga Mjini.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

| | JINA LA MAMLAKA YA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA | ENEO LINALOONGEZWA | |
|---|---|---|---|
| | | WILAYA YA MKINGA MKOA WA TANGA | |
| | MAMLAKA YA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA TANGA MJINI | KATA | KIJIJI |
| | | 1. Duga | 1. Horohoro border,<br>2. Horohoro Kijijini,<br>3. Mwakikoya,<br>4. Mwakikonge,<br>5. Maforoni. |
| | | 2.Parungu Kasera | 1.Parungu Kasera,<br>2.Mzingi Mwagogo,<br>3.Mkinga leo,<br>4.Gezani,<br>5.Manza,<br>6.Vuo,<br>7.Kipumbwi Magodi,<br>8.Magaoni,<br>9.Tawalani,<br>10.Mwandusi,<br>11. Mtundani,<br>12. Moa,<br>13.Zingibali<br>14.Boma. |
| | | 3. Maramba | 1. Maramba A,<br>2. Maramba B,<br>3. Matemboni,<br>4. Mbambakofi. |
| | | 4. Manza | 1. Manza,<br>2. Mwandusi,<br>3. Mtundani,<br>4. Tawalani. |
| | | 5. Boma | 1. Boma kichakamiba,<br>2. Boma subutuni, |
| | | 6. mkinga | 1. Mkinga leo,<br>2. Gezani,<br>3. magaoni. |
| | | 7. Moa | 1. Moa,<br>2. Vuo ‘B’ Mwachala,<br>3. Mwaboza, |

*Tangazo La Serikali Na. 195 (Linaendelea)*

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | 4. Zingibari. |

Dodoma,
11 machi, 2024

JUMAA H. AWESO
*Waziri wa Maji*